

SIKU YA KIMATAIFA YA TAFSIRI

SEMINA YA KAKAMA

Dhana

Tarehe 30 Septemba kila mwaka ni Siku ya Kimataifa ya Tafsiri (**Azimio la Umoja wa Mataifa 71/288**). Siku hii inatoa fursa kwa nchi, serikali, mashirika na watu binafsi duniani kote kusherehekea kazi ya wataalamu wa lugha na kutambua umuhimu wawingi-lugha. Tafsiri na ukalimani ni taaluma zinazohusiana na kutegemeana; zote ni muhimu kwa mawasiliano na maendeleo.

Ili kujiunga na kushirikiana na jamii ya watafsiri katika juhudi za kukuza taaluma ya tafsiri duniani, Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) inapanga kuwa na Semina ya **mtandaoni** siku ya Ijumaa, tarehe 29 Septemba, 2023 ili kuadhimisha umuhimu wa tafsiri na ukalimani wa Kiswahili katika ulimwengu wa tamaduni anuwai na wingi-lugha. Mada ya Semina hiyo ni **‘Kiswahili, Utu na Tafsiri’**.

Madhumuni ya Semina ni:

- Kusherehekea Kiswahili kama lugha kuu ya tafsiri na ukalimani;
- Kudhihirisha uwezo wa Kiswahili katika kufanikisha ajenda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia tafsiri na ukalimani;
- Kujadili umuhimu wa Kiswahili katika tafsiri na ukalimani duniani.

Washiriki wanaalikwa kuandaa na kuwasilisha ikisiri zisizozidi maneno 150 kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo au nyingine zinazohusiana nazo:

- Tafsiri na Ukalimani katika maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki
- Tafsiri na Fasihi
- Tafsiri na Ukalimani katika Vyombo vya Habari
- Tafsiri na Ukalimani katika Mahakama
- Tafsiri na Ukalimani na Uchumi-Bunifu
- Tafsiri, Ukalimani na Wingi-Lugha
- Tafsiri ya Kiswahili katika ufanikishaji wa Nadharia, Sera na Utendaji
- Tafsiri, Ukalimani na TEHAMA
- Taaluma za Tafsiri na Ukalimani
- Utafiti kuhusu Tafsiri na Ukalimani

Ikisiri ziwasilishwe kwa eakc-hq@eachq.org na nakala itumwe kwa phenry@eachq.org kufikia tarehe 4 Septemba, 2023.